







Hatua 12 za kuzingatia ili kupata mbegu bora ya mahindi isiyokuwa na Ugonjwa wa Mnyauko (Maize Lethal Necrosis-MLN)

Ugonjwa wa Mnyauko (Maize Lethal Necrosis-MLN) ni nini?

Ni Ugonjwa wa mahindi unaosababishwa na virusi. Ugonjwa huu husababishwa na muunganiko wa virusi vya aina mbili: Virusi vya Mabaka na Madoa ya Mahindi-Maize Chlorotic

Mottle Virus (MCMV) na mojawapo kati ya virusi vifuatavyo: Virusi vya Batobato ya Miwa-Sugarcane Mosaic Virus (SCMV), Virusi Vidumaza vya Batobato ya Mahindi-Maize Dwarf Mosaic

Virusi (MDMV) na Virusi Michirizi vya Batobato ya Ngano-Wheat Streak Mosaic Virus (WSMV)

- | | | | | | |
|--|--|--|---|---|--|
|  | 1 Pata historia ya shamba pamoja na ugonjwa katika shamba la kuzalishia mbegu kabla ya kupanda |  | 2 Hakikisha udongo una rutuba ya kutosha ili kuweza kupata mimea iliyo bora. Inashauriwa kupima rutuba ya udongo kila baada ya kipindi kisichozidi miaka mitatu ili kuweza kutambua aina ya mbolea itakayotumika |  | 3 Tumia mbegu iliyothibitishwa kutokwa na virusi vya ugonjwa wa Mnyauko katika kuzalisha mbegu. |
|  | 4 Safisha zana za kilimo kabla na baada ya kulima ili kuondoa uchafu unaoweza kuwa na virusi vya ugonjwa |  | 5 Panda mvua zinapoanza kunyesha ili kuepukana na ugonjwa |  | 6 Kagua shamba kila wakati ili kuweza kutambua kama kuna dalili za ugonjwa. Ondo nyasi, magugu na takataka zingine shambani zinazoweza kuhifadhi au kuficha virusi vya ugonjwa wa Mnyauko |
|  | 7 Thibiti wadudu wanaoneza virusi vinavyosababisha Ugonjwa wa Mnyauko kwa kupulizia viutilifu kwa kufuata utaratibu unaokubalika. |  | 8 Chunguza dalili za ugonjwa shambani, ng'oa, choma au fukia mimea yote itakayoonekana kuwa na dalili za ugonjwa nje ya shamba. |  | 9 Chukua sampuli za mimea itakayohisiwa kuwa na virusi, chunguza sampuli hizo kwenye baabara (au kwa kutumia kifaa maalum) ili kuthibitisha kama mimea hiyo ina ugonjwa. |
|  | 10 Baada ya kuvuna chagua magunzi pamoja na punje zenyet ugonjwa, viteketeze kwa kuvichoma moto. |  | 11 Pulizia mbegu viutilifu vinavyoshauriwa ili kuweza kuepukana na Ugonjwa wa Mnyauko |  | 12 Tumia kilimo cha mzunguko wa mazao (kwa kupanda mimea aina ya mikundekunde) angalau kila baada ya msimu mmoja |
- Dalili za Ugonjwa wa Mnyauko wa Mahindi**
- Madoadoa machache au mengi kwenye jani ambayo huanzia chini ya shina la jani changa na kusambaa kuelekea kwenye ncha yake.
 - Majani machanga hukauka kabla ya mmea kuchanua, hali hiyo husababisha dalili inayoitwa 'kifo cha moyo', hatimaye kifo cha mmea mzima.
 - Jani hukauka kuanzia kwenye kingo zake na kusambaa kuelekea katikati, hatimaye jani lote.
 - Mmea hudumaa na kukomaa kabla ya wakati wake.
 - Wakati mwagine mmea huwa tasa (hakuna utengenezaji wa chamvua).
 - Gunzi huwa na mbegu chache zilizohafifu au kutokwa na mbegu kabisa.
 - Maganda ya mhindi hukauka kabla hayajakomaa wakati sehemu zingine za mmea zikiwa bado ni mbichi (zikiwa na rangi ya kijani).
 - Gunzi huoza
 - Mashambulizi ya kuvu wenye rangi ya kijivu kwenye magunzi yaliyooza hujitokeza kama maambukizi nyemelezi
- Namna Ugonjwa wa Mnyauko unavyoonezwa**
- Ugonjwa wa Mnyauko hueneza kwa njia zifuatazo:
- Wadudu wa aina mbalimbali, wakiwemo: Vidukari na Vithiripi-hula kwa kufyonza utomvu wa mahindi; minyoo ya mizizi; panzi na mbawa kavu-hushambulia majani.
 - Wanyama wa aina mbalimbali, binadamu pamoja na zana za kilimo-katika kuzihamisha kutoka shamba moja hadi jingine (kunawenza kukawa na shamba lenye ugonjwa)
 - Hueneza pia na mbegu ila ni kwa kiasi kidogo



The Alliance for a Green Revolution in Africa (AGRA)
S.L.P. 66773. Westlands 00800
Nairobi, Kenya
Simu: +254 (20)3675 000
+254 703 033 000
Tovuti: www.agra.org



International Maize and Wheat Improvement Centre (CIMMYT)
Barua pepe: l.m.suresh@cgiar.org
Simu: +254 702 392 664
Tovuti: cimmyt.org



African Agricultural Technology Foundation (AATF)
S.L.P. 30709-00100, Nairobi, Kenya
Simu: +254 (0) 20-4223700
Barua pepe: aatf@aatf-africa.org
Tovuti: www.aatf-africa.org



Tanzania Agriculture Research Institute (TARI) Ukariguru
S.L.P. 1433, Mwanza, Tanzania
Simu: +255(28)2983 104, +255 735 983104
Barua pepe: cdukiriguru@tari.go.tz
Tovuti: www.tari.go.tz